



JAMHURI YA MUUUNGANO WA TANZANIA
OISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MTAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA



Unapojibu tafadhali taja
Kumb. Na. GDC/II.20/9/35



23/05/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Geita imepokea kibali cha kutekeleza ikama na Bajeti kwa Ajira mpya ya mwaka wa fedha 2021/ 2022 yenye Kumb. Na. 97/228/01/9 cha terehe **13 Mei, 2022** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Raisi Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita anawatangazia Wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa za kuomba nafasi zilizoordheshwa hapo chini.

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA III (NAFASI 14)

Sifa za Mwombaji

- Awe amefauli kidato cha Nne (IV) au kidato cha sita (VI)
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada (**Cheti**) "NTA Level 5" kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali katika fani zifuatazo
 - Utawala
 - Sheria
 - Elimu ya Jamii
 - Usimamizi wa Fedha
 - Maendeleo ya Jamii
 - Sayansi ya Jamii

Kazi na Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji

- Katibu wa kamati ya Halmashauri ya Kijiji
- Mtendaji Mkuu wa Kijiji
- Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Kijiji.
- Mshauri wa kamati ya Kijiji kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Kijiji.
- Msimamizi wa Utekelezaji wa Sheria ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Kijiji.
- Mshauri wa Kamati ya Kijiji kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
- Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika kijiji.

- Mshauri wa Kamati ya Kijiji kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
- Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika kijiji.
- Kusimamia ukusaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote katika Kijiji.
- Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Kijiji.
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

Mshahara

- Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Serikali, yaani **TGS B** kwa Mwezi.

2. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 4)

SifazaMwombaji

- Awe amefaulu kidato cha Nne (IV)
- Leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhulia mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (**Basic Driving Course**) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya ufundi stadi (**VETA**) au chuo kingine kinacho tambuliwa na Serikali.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

Majukumu ya kazi ya Udereva:

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ilikubaini hali ya usalama wa gari.
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- Kufanya usafi wa gari na
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyo elekezwa na Msimamizi wake.

Mshahara

- Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Serikali, yaani TGS B kwa Mwezi.


3. MASHARTI KWA UJUMLA

- Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na usiozidi miaka aroabaini na tano (45).
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Waombaji waambatanishe maelezo yao binafsi (C.V)
- Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha IV au VI, cheti cha kuzaliwa na picha moja ya rangi katika barua ya maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.
- "Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya matokeo ya kidato cha Nne na sita(FORM IV and FORM VI RESULT SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wa husika watachukuliwa hatua za kisheria.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 06/06/2022 saa 9:30 alasiri.


Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Geita,
S.L.P 139,
GEITA.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:


John P. Wanga

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**



Nakala: Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
DODOMA.

Mbao za matangazo.